

Vyombo vya habari vyenye malengo

Hapana shaka kuwa nafasi ya vyombo vya habari duniani ni muhimu sana na tendaji kubwa na wala haiwezekani kuvizembea na kuvipuuzia, na vyombo vya habari vyenye malengo ni vile vyenye kujenga na sio vile vyenye kubomoa.

Na hakuna yeyote apingaye kuwa vyombo vya habari vya kisasa vinapita katika mikondo tafauti, baadhi yake vinajishughulisha na masuala ya kitaifa, vyengine vya kisiasa sawa imechama tawala au upinzani, viko pia visivyomili upande wowote au vya kuajiriwa na baadhi ni vya biashara na vyengine ni vya kijamii na kibinafsi.

Na kila chombo kinapimwa kutokana na kazi zake zifanyazo kwa jamii na kujiweka kwake katika kufuata misingi ya kikazi na maadili ya kiutangazaji, na kuacha kumili pamoja na kujadili mambo kwa kina na kwa mitazamo ya viongozi na waandishi wake na wasomi wake pamoja na wahabari wake pia kuzingatia ubora wa wafanyakazi wake katika fani hiyo.

Na nilazima kwa kila taasisi ya utangazaji au isiyo ya utangazaji iwe na chombo cha uchunguzi ambao utachunga namna za ubora wa wafanyakazi wake katika kila sekta zake, kitu kitakachopelekea kuzidisha ufanisi na uwezo wake wa kuweza kushindana na vyombo vya habari sawa viwe vya kitaifa au vya kimataifa. Na kikusudiwacho ni ufuatiliaji wa kweli wenye hisia za kitaifa na dhamiri ya kikazi.

Na hapana shaka kuwa ulimwengu wa kimaarifa upo wazi zaidi na una uwezo mkubwa wa kujipambanua, na kuweza kumjua nani mwenye ujuzi wa kazi hii na nani asiye na ujuzi wa kazi hii (ya utangazaji) kwa kuwa ni kazi yenye kuhitaji uwezo wa kifikra na maarifa.

Na hakuna shaka kuwa taasisi za magazeti ya kitaifa yamesaidia kwa kiwango kikuba katika kurekebisha mwenendo wa utangazaji na ushirikiano wake wa kutoa huduma katika kujadili masuala ya kitaifa. Na kuzifanya taasisi hizi kuwa na heshima kubwa kwa wananchi kwa ujumla na kwa wasomi kwa kuwahusisha wao pekee.

Na hapana shaka pia mikutano ya kiuchumi na ya kisomi ambayo inafanywa na baadhi ya taasisi za magazeti makubwa ni mojawapo ya shajiisho kubwa lenye kustahiki pongezi na hongera. Vilevile kuzingatia masuala ya kisomi na uchambuzi wa kina kwa kusaidia kuweka wazi sura na mitazamo. Na pengine hata fikira zilizo nje ya sanduku kuziweka wazi mbele ya watengenezao maamuzi.

Pamoja na kuweka wazi tafauti kati ya uhakiki ambao unakusudia kubomoa na uhakiki wa maudhui ambao huleta nyongeza kubwa sana katika Nyanja za kisomi nakitamaduni na kiidara na kiuchumi nacho ni kitu ambacho kinahitajika tukikaribishe sote na kukishajiisha na tufaidike nacho. Na kuona kuwa ni nyongeza isiyo na upungufu ilivyokuwa inachunga misingi ya kazi na masilahi ya taifa.

Na kumiliki hisia za kutosha za kupanga mambo, na katika mambo ya kuzingatia pia ni kuendesha mafunzo ya vizazi virithishane . Na wale wenye ujuzi wa kazi wawafunze vijana na kuwajuvya uhumimu wa kuwasiliana na mazungumzo yenye kuendelea kati ya wahusika na waandishi wa habari (wanahabari), na kuwepo na uhusiano uliokamilika wenye kuwa na masilahi ya kitaifa pamoja na kuhakikisha

umaridadi. Na kama alivyosema mmoja wa waandishi wa habari” “ nimejifunza kutoka kwa walimu wangu kuwa ni afadhali kuzikosa habari mia moja kuliko kupoteza ukweli wangu katika kueneza habari moja kwa njia isiyo sahihi.